

Wapendwa Wazazi,

Mapema msimu wa kichipua mwaka 1820, karibu na wakati wa Pasaka, Joseph Smith aliomba na kuwaona Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo. Gazeti hili linazungumza kuhusu wakati huo maalum. Hizi ni kurasa cha-che za kutafuta:

- Hadithi inayosimuliwa kwa picha inaelezea jinsi ambavyo Kanisa Lililorejeshwa ni sehemu ya mpango wa Mungu (R4–10).
- Rais Nelson anatueleza jinsi ambavyo tunaweza kutoa msaada kwa Urejesho (R2).
- Wimbo mpya unafundisha kuhusu Ono la Kwanza (R16–17).
- Hadithi inafundisha jinsi Urejesho unavyoweweza kubariki familia zetu (R20–21).

Je, si inapendeza kwamba tunaweza kuwa wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho? Acheni tushiriki habari njema ya Yesu na Kanisa Lake kwa ulimwengu!

Pasaka Njema,

Rafiki

JINSI YA KUTUMA KAZI YA SANAAYA MTOTO WAKO AU UZOEFU KWENYE LIAHONA

Nenda kwenye liahona.ChurchofJesusChrist.org na bofya "Wasilisha Makala au Majibu." Au itume kwetu kupitia barua pepe liahona@ChurchofJesusChrist.org likiwemo jina la mtoto wako, umri, jiji la makazi; na maelezo haya ya ruhusa: "Mimi, [ingiza jina lako], natoa ruhuso kwa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho kutumia wasilisho la mtoto wangu kwenye magazeti ya Kanisa, kwenye mitandao ya Kanisa na kwenye majukwaa ya mitandao ya kijamii, na yamkini katika nyenzo zingine za Kanisa." Tuna hamu ya kusikia kutoka kwako!



Tafuta Liahona iliyofichwa ndani!

YALIYOMO

- R2** Kutoka kwa Urais wa Kwanza:
Kutoa Msaada kwa Urejesho
- R4** Kanisa la Yesu Kristo Limerejeshwa!
- R11** Vitu vya Kuburudisha: Itafute!
- R12** Ukurasa wa Kupaka Rangi
- R14** Kanisa kwa ajili ya Zulma
- R16** Muziki: Ono La Kwanza
- R18** Hujambo kutoka katika Msitu Mtakatifu!
- R20** Familia ya Milele ya Alonso
- R22** Hekalu na Wewe
- R23** Wazo Zuri